# BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## ULIPAJI WA ADA YA MWAKA YA WANACHAMA WA PSPTB

**Dodoma Septemba 14, 2025.**

Bodi ya wataalamu wa ununuzi na ugavi (PSPTB) ni taasisi ya serikali iliyop chini ya wizara ya Fedha, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya PSPTB Sura ya 179 ya Sheria za Tanzania. PSPTB ni chombo cha kisheria chenye mamlaka ya kusimamia na kudhibiti viwango, mwenendo na maadili ya taaluma ya ununuzi na ugavi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 7(g) cha Sheria ya PSPTB, Bodi imepewa mamlaka ya kipekee ya kusajili watu waliokidhi vigezo na kuwapa mamlaka ya kisheria ya kufanya kazi kama Wataalam wa Ununuzi na Ugavi. Mtu yeyote ambaye hajasajiliwa rasmi kwa mujibu wa sheria hii, hana uhalali wa kushiriki au kufanya kazi za ununuzi na ugavi.

Kwa mujibu wa Kanuni za PSPTB, Tangazo la Serikali Na. 364 la mwaka 2009, na masharti mengine ya Sheria ya PSPTB, kila mtaalamu aliyesajiliwa anawajibika kisheria kulipa ada ya mwaka kila mwaka kama itakavyowekwa na Bodi.

Mtaalam yeyote atakayeshindwa kulipa ada hiyo kwa kipindi cha miezi ishirini na minne (24) mfululizo, atachukuliwa kuwa amepoteza hadhi yake ya usajili, na jina lake linaweza kuondolewa kwenye daftari rasmi la usajili la PSPTB.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 46(2) na (3) cha Sheria ya PSPTB, mtu yeyote atakayeendelea kufanya kazi, kujitambulisha au kujihusisha na taaluma ya Ununuzi na Ugavi bila kusajiliwa na PSPTB, anafanya kosa la jinai linalostahili adhabu kwa mujibu wa sheria, na Bodi inatachukua hatua za kisheria na kinidhamu bila taarifa nyingine yoyote kama ilivyoelewa na Kanuni za maadili na mwenendo za wataalamu wa ununuzi na ugavi Tangazo la Serikali Na. 365 la mwaka 2009 (PSPTB Code of ethics and Conducts).

*Mkandarasi Place (Ghorofa ya Saba), S.L.P. 2663 ,Msimbo wa Posta 41108 Dodoma. Simu: + Nukushi: +*
*Tovuti:http://www.psptb.go.tz. Barua pepe: barua@psptb.go.tz*

**HATUA UNAYOTAKIWA KUCHUKUA KWA SASA.:**

Wataalam wote ambao bado hawajalipa ada zao wanatakiwa kulipa madeni yote ya ada ya mwaka ndani ya siku **30** tangu tarehe ya kutolewa kwa tangazo hili. Kutotekeleza agizo hili kutasababisha kufutwa mara moja kwa usajili wenu, na majina yenu yatachapishwa rasmi. Hatua zaidi za kisheria zinaweza kuchukuliwa, ikiwa ni pamoja na kufunguliwa mashitaka kwa mujibu wa sheria iliyoianzisha PSPTB.

**Imetolewa na:-**

Godfred B. Mbanyi

**Mkurugenzi Mtendaji - PSPTB**